

# Muhtasari wa Kipindi cha Usajili

## Mafao ya 2026

HelloFresh inatambua kwamba wafanyakazi wetu ndio rasilimali yetu ya thamani zaidi na tunajitahidi kuwekeza katika ustawi wenu. Mpango wetu wa kina wa mafao umekusudiwa kukidhi mahitaji yako ya kipekee, kushughulikia suala la uwezo wa kumudu gharama na kusaidia kila mtu anayefanya kazi katika HelloFresh. Tunatoa aina mbalimbali za mafao ili kukusaidia kuwa na afya njema, kuhisi salama na kufanikisha malengo yako.

HelloFresh inafanya mabadiliko kadhaa kwenye mpango huu kuanzia mwaka wa 2026 na tunatoa nyenzo za kukusaidia katika mchakato wa usajili. Unapaswa **kukagua taarifa zilizoambatanishwa** ili kupata muhtasari na **uchanganue msimbo wa QR ulio hapo chini ili kufikia Mwongozo wa Mafao na Tovuti ndogo**. Pia utaweza **kupanga muda wa kukutana na washauri wa usajili ana kwa ana kituoni kwako katika wiki zijazo**.

**Sharti ushiriki katika mchakato wa Usajili wa Workday ili kuhakikisha kuwa umejisajili kwa bima ambayo ungependa kwa mwaka wa 2026.**

## Nini Kipya!

- HelloFresh itatoa chaguo la 3 la mpango wa matibabu: Mpango wa Malipo ya Mshiriki wa Open Access Plus (OAP) wenye Akaunti ya Fidia ya Afya (HRA): Makato ya $5,000, kiwango kinalingana na kiasi kinachotolewa na mwajiri na malipo ya mshiriki kwa ajili ya huduma. HelloFresh italipia asilimia 100 ya kiasi unachopaswa kutoa kutoka kwa mshahara wako kwa bima ya mfanyakazi pekee.
- HelloFresh pia itatoa mpango wa 2 wa huduma za meno: chaguo la Msingi (Base) na Lililoboreshwa (Buy-Up) na tutaendelea kulipa sehemu ya ada ya kununua bima hiyo.
- HelloFresh itagharamia asilimia 100 ya uchunguzi wa kuzuia magonjwa ya ngozi katika mpango wa HRA na wa Malipo ya Kawaida ya Mshiriki. Katika Mpango wa Afya Wenye Makato ya Juu (High Deductible Health Plan, HDHP) wenye HSA, huduma zitalipiwa kwa asilimia 100 baada ya makato kulipwa.
- Bima ya Maisha pamoja na Huduma za Muda Mrefu kupitia Allstate/Standard.
- Bima ya Kisheria kupitia MetLife.

## Mabadiliko Muhimu!

- Pesa zitahitaji kukatwa kutoka kwenye mshahara kwa mipango yote ya bima ya afya na viwango vyote vya bima isipokuwa kwa bima ya mfanyakazi pekee katika Mpango wa Malipo ya Mshiriki wa OAP wenye Akaunti ya Fidia ya Afya (HRA). HelloFresh italipia huduma za afya za mtandaoni (MDLive) kwa asilimia 100 katika mipango yote ya bima ya afya.
- Bima iliyoboreshwa ya Ulemavu wa Muda Mrefu na Bima ya Hiari ya Maisha zitapatikana moja kwa moja wakati wa Usajili kwa wafanyakazi wote wanaotimiza masharti.
- Mpango wa Afya wenye Makato ya Juu (High Deductible Health Plan, HDHP) wenye mpango wa Akiba za Afya (Health Savings Account, HSA): Kiasi cha makato na malipo unayolipa mwenyewe kimeongezeka hadi kiasi kisichozidi $3,400. Sasa kutakuwa na makato ya ada ya kununua bima kutoka kwa mshahara kwa viwango vyote vya bima.
- Pesa zinazotolewa kila mwezi za kulipia mpango wa Bima ya Huduma za Macho zitagharamiwa kwa asilimia 100 na mfanyakazi.

Ikiwa hutashiriki katika Kipindi cha Usajili na kwa sasa uko kwenye Mpango wa Malipo ya Kawaida ya Mshiriki wa OAP : Makato ya $1,000, bima yako ya sasa itahamishwa moja kwa moja hadi kwenye Mpango wa HDHP. Tazama kurasa za 2–3 kwa maelezo zaidi.

HELLO FRESH

**Changanua hapa**
ili kukagua Mwongozo wa Mafao na Tovuti ndogo kwa maelezo zaidi ya mafao yaliyoelezwa hapa.



# Ni Hatua Gani Ninazohitaji Kuchukua?

**Muhimu!Ni SHARTI ushiriki katika Kipindi cha Usajili cha mwaka huu. Ikiwa hutachagua mpango wowote, bima yako ya sasa ya afya itahamishwa moja kwa moja hadi kwenye Mpango wa Bima ya Afya wa HDHP na Mpango wa Huduma za Meno wa Base kwa ajili yako na wategemezi wako.** Hata kama hutaki kufanya mabadiliko yoyote kwenye mafao yako, tunakuomba ukamilishe mchakato wa usajili ili kuhakikisha kuwa taarifa zako na za wategemezi wako ni sahihi, uthibitishe kwamba umekubali bima ya chaguo msingi na ujisajili au kujisajili upya kwenye Akaunti ya Matumizi Mbalimbali kwa Huduma za Afya (Flexible Spending Account, FSA).

Kipindi cha Usajili ndio wakati wa pekee wa mwaka ambapo unaweza kufanya mabadiliko ya mafao yako. Ukikosa kufanya mabadiliko katika kipindi cha Usajili kuanzia **Novemba 5, 2025, hadi Novemba 18, 2025**, hutaweza kufanya mabadiliko tena baadaye isipokuwa utakapokuwa na tukio la maisha linalostahiki. Mabadiliko sharti yafanywe kwenye Workday ukiwa na hati za uthibitishaji (k.m., cheti cha kuzaliwa, cheti cha ndoa, n.k.) ndani ya siku 31 baada ya matukio ya maisha kutokea.

- Kagua nyenzo zako za usajili wa mwaka 2026 katika **benefitsgo.com/hellofresh**.
- Ili kufanya uchaguzi wako katika Kipindi cha Usajili:
  - **Mtandaoni**: Ingia kwenye **https://wd103.myworkday.com/hellofresh/login.htmld** (au utumie programu ya simu ya Workday)
  - **Piga simu kwa**: HelloFresh Benefits and Payroll Connect kwa nambari **1-877-431-7867** (Jumatatu hadi Ijumaa saa 8 asubuhi hadi 5 jioni CST; tafsiri inapatikana)

  **Kuanzia tarehe 5 Novemba** unaweza kujisajili kwa mara ya kwanza, kufanya mabadiliko kwenye uchaguzi wako wa sasa, kuchagua mafao mapya ya hiari, au kuchagua upya FSA ya Huduma za Afya au FSA ya Huduma za Wategemezi kwa mwaka wa 2026.
- Ili kujaza fomu ya Kipindi cha Usajili, utahitajika kuongeza au kusasisha taarifa za wanufaishwa wako kwenye Workday. Utahitaji jina, nambari ya simu, anwani na hali ya uhusiano.
- Jaza na uwasilishe fomu yako ya usajili kufikia Novemba 18, 2025. **Hutaruhusiwa kufanya mabadiliko yoyote** baada ya Novemba 18, 2025.
- Unapaswa kuhifadhi uthibitisho wa mafao yako kwa kumbukumbu zako kwa kuchapisha, kuhifadhi, au kupiga picha ya skrini au picha kwa kutumia simu yako, kwa sababu hautatumiwa uthibitisho kwa njia ya barua pepe.

Mabadiliko ya chaguo la mpango wa 401(k) yanaweza kufanywa wakati wowote ndani ya mwaka kwa kuingia kwenye akaunti yako katika **voyaretirementplans.com** au kwa kutumia programu ya Voya Retire. Je, bado hujajisajili? Jisajili leo kwa kutembelea **enroll.voya.com** au kupiga simu kwa nambari **1-888-311-9487**. Tumia Nambari ya Mpango: **551637** na Nambari ya Uthibitishaji: **55163799** ili kujisajili.

## Muda wa Mwisho wa Kufanya Usajili

| Aina ya Mfanyakazi/Mtegemezi | Nafasi ya Usajili | Tarehe ya Bima Kuanza Kutumika |
|---|---|---|
| **Mfanyakazi wa Sasa** | Wakati wa Kipindi cha Usajili kuanzia Novemba 5, 2025 hadi Novemba 18, 2025. | Januari 1, 2026 |
| **Mfanyakazi Mpya** | Kutakuwa na vipindi viwili vya usajili kwa wafanyakazi wapya watakaoanza kufanya kazi kati ya Novemba 5, 2025 na Desemba 31, 2025 kwa ajili ya uchaguzi wao wa mwaka wa 2025.<br>Baada ya usajili wa wafanyakazi wapya kukamilika na kuchakatwa, utahitajika kukamilisha hatua ya Kipindi cha Usajili ndani ya wiki mbili kwa ajili ya uchaguzi wa mwaka wa 2026. | |
| **Mfanyakazi Aliyekumbwa na Tukio la Maisha Linalostahiki (QLE)** | Baada ya usajili wa tukio la maisha kukamilika na kuchakatwa, kwa QLE zitakazofanyika mwaka wa 2025 na kuchakatwa baada ya Novemba 5, 2025, utahitajika kukamilisha hatua mpya ya Kipindi cha Usajili ndani ya wiki mbili kwa ajili ya uchaguzi wa mwaka wa 2026. | |

# Muhtasari wa Mafao ya 2026

| Aina ya Mafao | Je, Uchaguzi Wako wa 2025 Utaendelea Kutumika kwa Mwaka wa 2026? | Je, Unahitaji Kuukagua? | Unahitaji Kuchaguliwa na Mfanyakazi | Unatolewa na HelloFresh |
|---|---|---|---|---|
| **Bima ya Matibabu/Dawa (Rx)** | **Unahitaji kuchukua hatua - ikiwa hutachagua chaguo lolote mwaka huu, mpango wako wa sasa utahamishwa moja kwa moja hadi Mpango wa HDHP.** | X | X | |
| **Matibabu ya meno** | **Unahitaji kuchukua hatua - Ikiwa hutachagua chaguo lolote mwaka huu, mpango wako wa sasa utahamishwa moja kwa moja hadi Mpango wa Base Dental Plan** | X | X | |
| **Matibabu ya macho** | Ndiyo | X | X | |
| **Akaunti ya Akiba za Afya (HSA)** | Ndiyo | X | X | |
| **Akaunti ya Matumizi Mbalimbali kwa Huduma za Afya** | **Unahitaji kuchagua chaguo jipya** | X | X | |
| **Akaunti ya Matumizi Mbalimbali kwa Huduma za Wategemezi (FSA)** | **Unahitaji kuchagua chaguo jipya** | X | X | |
| **Bima ya Hiari ya Ajali, Magonjwa Hatari, na Fidia ya Kulazwa Hospitalini** | Ndiyo | X | X | |
| **Akaunti ya Gharama za Usafiri** | Ndiyo | X | X | |
| **Akaunti ya Gharama za Maegesho ya Wafanyakazi** | Ndiyo | X | X | |
| **Mafao ya Bima ya Msingi ya Maisha na AD&D** | Ndiyo | X | | X |
| **Mafao ya Bima ya Hiari ya Maisha na AD&D kwa Mfanyakazi, Mwenzi wa Ndoai na Mtoto/Watoto** | Ndiyo | X | X | |
| **Ulemavu wa Muda Mfupi** | Ndiyo | X | | X |
| **Ulemavu wa Muda Mrefu** | Ndiyo | X | | X |
| **Mafao ya Bima Iliyoboreshwa ya Ulemavu wa Muda Mrefu** | Ndiyo | X | X | |
| **Mpango wa Kustaafu wa 401(k)** | Ndiyo | X | X | |
| **Mpango wa Usaidizi kwa Wafanyakazi (EAP)** | Huhitaji Kuchagua Chaguo Lolote | X | | X |
| **Huduma ya Muda Mfupi ya Kutunza Watoto na Wazee** | Huhitaji Kuchagua Chaguo Lolote | X | | X |
| **Mafao ya Kusaidia Kuokoa Pesa kwa Gharama za Bili za Matibabu** | Huhitaji Kuchagua Chaguo Lolote | X | | X |
| **Bima ya Maisha yenye Huduma za Muda Mrefu** | **Unahitaji kuchagua chaguo jipya** | X | X | |
| **Bima ya Ulinzi Dhidi ya Wizi wa Utambulisho** | **Unahitaji kuchagua chaguo jipya** | X | X | |
| **Bima ya Kisheria** | **Unahitaji kuchagua chaguo jipya** | X | X | |

## Tembelea Tovuti yetu kwa taarifa zaidi.

Pamoja na Hati hii ya Muhtasari, **benefitsgo.com/hellofresh** ni tovuti unayoweza kupata taarifa zote kuhusu Kipindi cha Usajili kwa mafao yote yanayotolewa kwako, ikiwa ni pamoja na taarifa kama vile vipeperushi vya watoa huduma na video zitakazokusaidia wewe na familia yako kufanya maamuzi kuhusu mafao yako ya mwaka 2026.

Pia unaweza kufikia **MyHelloFreshBenefits.com** kwa taarifa zaidi wakati wowote. Huhitaji kufungua akaunti, na tovuti hii inaweza kufikiwa kupitia kompyuta, kompyuta kibao au simu ya mkononi wakati wowote. **Tafadhali kumbuka, kuna menyu kunjuzi kwenye kona ya juu kushoto ya ukurasa wa mwanzo ambapo unaweza kuchagua lugha unayoipendelea.**

# Taarifa Zaidi Kuhusu Akaunti za Mpango wa Afya

## Mpango wa Fidia ya Afya (Health Reimbursement Plan, HRA) ni nini?

Mpango wa HRA, au Akaunti ya Fidia ya Afya, ni mafao yanayotolewa na mwajiri ambapo mwajiri hufidia mfanyakazi gharama zinazohusiana na matibabu zilizostahili. HRA husaidia kupunguza gharama unazolipa mwenyewe za huduma za afya na hukupa uhuru zaidi wa kudhibiti gharama za matibabu.

Ikiwa mfanyakazi atachagua mpango huu, HRA hutoa malipo ambayo mfanyakazi angelipa kwa gharama zozote za makato au malipo yanayostahili kulipwa na mshiriki, kwa matibabu na dawa. Huhitaji kuwasilisha madai ya fidia. Mwajiri wako huweka pesa kwenye akaunti hii, na unaweza kuzitumia kulipia huduma kama miadi ya daktari, dawa, au gharama nyingine za afya.

Ikiwa umejisajili kwenye mpango wa mtu mmoja pekee, HelloFresh hufadhili HRA kwa $100. Ikiwa umejisajili kwenye kiwango kinachojumuisha wategemezi, kiasi kinachotolewa ni $200. Pesa katika HRA yako hutolewa na kampuni—hakuna makato kutoka kwa mshahara wako.

***Tafadhali kumbuka**pesa hazihamishwi kutoka mwaka mmoja hadi mwingine iwapo hutazitumia zote ndani ya mwaka mmoja. Baada ya pesa kuisha, utawajibikia gharama nyingine zote kwa kipindi kilichobaki cha mwaka.*

## Akaunti ya Akiba za Afya (HSA) ni nini?

HSA ni akaunti ya akiba yenye mafao ya ushuru inayoweza kukusaidia kuokoa pesa kwa gharama zako za huduma za afya zinazostahiki. Akaunti hii hukuruhusu kutenga pesa kabla ya ushuru ili kulipia gharama za huduma zinazotimiza masharti, ikiwa ni pamoja na makato, kiasi maalum cha pesa unacholipa unapopokea huduma na asilimia ya gharama za matibabu ambazo mfanyakazi anahitajika kulipa.

Ili kustahiki kuchangia kwenye Akaunti ya Akiba za Afya (HSA), sharti uwe umejisajili kwenye mpango wa makato ya juu (HDHP), usiwe umejisajili kwenye Medicare au TRICARE, usiwe na mpango mwingine wa bima usio wa HDHP, usiwe umeorodheshwa kama mtegemezi kwenye marejesho ya ushuru ya mtu mwingine na usiwe unapata bima kupitia mpango wa FSA au HRA kwa afya ya jumla.

| Je, unaweza kutoa kiasi gani cha pesa? | Kikomo cha Kiasi Kinachotolewa cha IRS kwa Mwaka wa 2026* |
|---|---|
| **Bima ya Mtu Binafsi:** | $4,400 |
| **Bima ya Familia:** | $8,750 |

**Watu wenye umri wa miaka 55 au zaidi wanaweza kutoa $1,000 za ziada ili "kuweka akiba ya baadaye".*

## Ni Mpango Upi Unakufaa Zaidi?

| Mpango wa Malipo ya Mshiriki wa Open Access Plus (OAP) wenye Akaunti ya Fidia ya Afya (HRA) | Mpango wa Malipo ya Kawaida ya Msiriki wa Open Access Plus (OAP) | Mpango wa Afya wenye Makato ya Juu (HDHP) wenye Akaunti ya Akiba za Afya (HSA) |
|---|---|---|
| Una kiasi cha juu zaidi cha makato ($5,000), lakini mwajiri wako hukupa Akaunti ya Fidia ya Afya (HRA) ya kurejesha gharama za aina zote. Ukiacha kazi, unapoteza pesa za HRA ambazo hukutumia. | Una kiasi cha chini zaidi cha makato ($1,000), na malipo maalum unayolipa kwa ziara za ofisini kwa daktari na dawa huanza mara moja. Hakuna HSA au HRA. Kwa kawaida, michango ya mfanyakazi kutoka kwenye mshahara huwa ya juu, lakini gharama unazolipa mwenyewe huwa za chini kabla ya asilimia ya gharama za matibabu ambayo mfanyakazi anahitajika kulipa kutozwa. | Utalipa kiasi cha juu cha makato ($3,400) na kugharamikia huduma zote kikamilifu hadi umalize kupia kiasi hicho chote cha makato. Baada ya hapo, mpango hugharamia sehemu kubwa ya gharama zako. Unaweza pia kuchangia kwenye Akaunti ya Akiba za Afya (HSA) kwa kutumia pesa zisizotozwa ushuru na utabaki na pesa hizo - hata ukibadilisha kazi. |